



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI



*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb.Na. HW/F.2/18/VOL VI/121

20 Septemba, 2022

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA VIBARUA WA KUKUSANYA  
MAPATO YA HALMASHAURI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni anawatangazia nafasi ya kazi ya Vibarua wa kukusanya mapato ya Halmashauri na anakaribisha maombi kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi hiyo kama ifuatavyo:

**SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe Mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.
- Awe raia wa Tanzania
- Awe na Elimu kuanzia Kidato cha Nne (IV) na kuendelea
- Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45.
- Awe na uwezo wa kutumia simu janja
- Awe tayari kufanya kazi eneo lolote katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni
- Awe mwadilifu

**KAZI NA MAJUKUMU YA MKUSANYA MAPATO**

- i. Kukusanya mapato ya Halmashauri
- ii. Kuwasilisha fedha benki baada ya kukusanya
- iii. Kuwasilisha taarifa ya ukusanyaji wa Mapato kwa Mweka Hazina Wilaya

**MASHARTI YA KAZI/WAOMBAJI KWA UJUMLA**

- Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na yatumwe kwa njia ya posta au kuwasilishwa moja kwa moja katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni sehemu ya Masijala ya Wazi kwa anuani ifuatayo:

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
S.L.P 60,  
MANYONI.**

- Barua ziambatishwe na:-
  - Nakala ya cheti cha elimu ya kidato cha nne na kuendelea
  - Nakala ya cheti cha kuzaliwa
  - Nakala au Namba ya kitambulisho cha NIDA
  - Maelezo binafsi yenye majina na namba za simu za wadhamini wasiopungua wawili
  - Barua ya utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa kijiji au Kata husika
  - Picha mbili (2) ndogo (Passport size) za hivi karibuni
- Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi zitapelekea wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria.
- Waombaji watakaokidhi sifa ndio watakao itwa kwenye usahili.
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **27/09/2022** Saa **9:30** alasiri. Tangazo pia linapatikana kwenye **mbao za matangazo** na tovuti ya Halmashauri **www.manyonidc.go.tz**.

Tangazo hili limetolewa na;



Melkizedeck Oscar Humbe

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI**